

**Learning on TAP**

# Teknolojia saidizi

## Maneno muhimu: Vifaa saidizi vya usikivu viliyosetiwa tayari

| Neno | Maana | Picha |
|---|---|---|
| **Apu** | Kifupisho cha neno linalomaanisha programu.  Ni kifaa cha kidigitali kinachotumika kwenye simu au kishikwambi kufanya kazi maalumu. | |
| **Odiogramu** | Ni chati ya usikivu alionao anayepimwa inaonyesha sauti ya chini kabisa ambayo mhusika anaweza kusikia (kiwango cha mwisho cha sauti) katika mafasa tofauti ya sauti. |   |
| **Odiomita** | Kifaa cha kupima usikivu |   Apu ya odiomita iliyoko kwenye kishikwambi |
| **Odiometri** (Kipimo cha usikivu) | Kipimo kinachoonyesha ni kwa namna gani mhusika anaweza kusikia. Kama kuna upotevu wa usikivu, matokeo yataonyesha kiwango cha upotevu huo. | |
| **Wastani wa kiwango cha sauti cha chini kabisa ambacho mhusika anaweza kusikia** | Jumla ya viwango vya sauti vya chini kabisa ambavyo mtu anayepimwa anaweza kusikia vya 500 Hz, 1000 Hz, 2000 Hz, na 4000 Hz halafu kugawa idadi kwa nne. | |
| **Mtaalamu wa masikio na usikivu** | Wataalamu ambao hupima, husimamia na kutibu matatizo ya masikio na usikivu. | |
| **Mwangwi** (Mluzi) | Sauti ya "filimbi" kutoka kwenye kifaa saidizi cha kusikia pale ambapo sauti inapenyeza kutoka kwenye sikio na kupokelewa na kipaza sauti cha kifaa saidizi cha kusikia. | |
| **Masafa** | Ni mara ngapi  mawimbi ya sauti yanasafiri juu na hcini ndani ya sekunde moja. Kuna aina tofauti za sauti ikiwepo sauti nzito ( masafa ya chini) kama vile sauti ya ngoma na vitu vilivyonolewa (masafa ya juu) kwa mfano filimbi. Masafa yanapimwa kwa Hezi (Hz) |   |
| **Kusikia kwa taabu** | Neno linalotumika kwa mtu ambaye ana upotevu wa kusikia kwa **kiasi** hadi **kikubwa** ambaye hawezi kusikia vizuri kama mtu mwenye usikivu wa kawaida. | |
| **Sauti ya chini kabisa ambayo inaweza kusikika** | Sauti ya chini kabisa ambayo mgonjwa anaweza kusikia katika masafa tofauti ya sauti. | |
| **Hezi** (Hz) | Namna ya kupima idadi ya mara ngapi kitu kinatokea ndani ya sekunde moja. Kwa mfano, kama mawimbi ya sauti | |

| | | |
|---|---|---|
| | yanatetemeka mara 100 ndani ya sekunde moja, yana masafa ya Hz 100. | |
| **Sauti za Lingi** | Seti ya sauti sita.<br>Sauti hizi huchukua wigo wote wa sauti za maongezi kwa masafa ya chini hadi masafa ya juu |  |
| **Kifinyazi cha sikio kilichotengenezwa kwa ukubwa uliozoeleka** | Sehemu ya kifaa saidizi cha kusikia ambayo imetengenezwa tayari katika ukubwa tofauti ili kuweza kutosha kwenye sikio la mhusika. Inaunganisha na kifaa saidizi cha kusika kwa kutumia bomba na hufikisha sauti kwenye sikio la mtumiaji. |  |
| **Stetoklipu**<br>(Bomba la kusikiliza) | Inajulikana vilevile kama bomba la kusikiliza. Linamruhusu mtumiaji mwenye usikivu wa kawaida kufuatilia kujua kama kifaa saidizi kinafanya kazi vizuri. |  |